**Learning by Ear 2011/2012 – Corruption – The Elephant in the Room**

**Episode 08 – "A Whistleblower in the Family"**

**Text: Victoria Averill**

**Editing: Johannes Beck, Friederike Müller, Pendo Paul**

**Proofreading: Charlotte Collins, Pendo Paul**

**Kisuaheli: Eric Ponda**

CHARACTERS:

- NARRATOR

Scene 1:

- Jennifer (FEMALE, 55)
- Alfayo (MALE, 58)
- Waiter (MALE, around 30)
- NARRATOR

Scene 2:

- Lydia (FEMALE, 16)
- Tekla (FEMALE, 16)
- Sylvia (FEMALE,19)

- Journalist 1 (FEMALE, 30)
- Journalist 2 (MALE, 30)
- Jeffrey (MALE, 58)

Scene 3:

- TV Anchor/Newsreader (FEMALE, 40)

**Intro:**

**0. Narrator:** Hujambo na karibu katika makala ya nane kwenye mfululizo wa vipindi vya " **Noa Bongo Jenga Maisha yako**" tukiwa bado tunazungumzia suala la ufisadi, kwenye mchezo huu "**Tembo Nyumbani**" .

Katika kipindi kilichotangulia Lydia na rafiki yake Tekla, kwa ujasiri wao wamemrekodi sauti mwalimu wao akikiri kupokea hongo. Naye Jeffrey Thiongo anaamua kujitosa katika ulingo wa siasa kwenye uchaguzi mkuu ili kupata fursa nzuri zaidi ya kupambana na ufisadi ndani ya serikali.

Katika kipindi cha leo "**Mpinga Kipenga Alfayo Odhiambo**, hatimaye anaamua kumueleza Mkewe Jennifer, kuhusika kwake kwenye sakata la nishati. Na Je, vyombo vya habari

vitakuwa na hamu ya kufahamu ufisadi unaoendelea shuleni? Endelea kusikiliza!

## Scene One:

**1. Atmo:** **Restaurant noise**

**2. Jennifer:** Ah Alfayo, nimefurahia sana kwa mualiko huu. Ni siku nyingi tangu sisi wawili kula pamoja chakula cha jioni mgahawani. Nimefurahi sana kwa mualiko huu!

***KW begin*** Utakula nini? Ninapenda wali na kuku wa kuchoma, mate yanameanza kunidondoka. Na wewe?

**3. Alfayo:** Mmm. Sina hakika. Kwanza nataka kuagiza vinywaji, utakunywa *Wine*, Jennifer?

**4. Jennifer:** Napenda sana. *White Wine* tafadhali.

***KW end***

**5. Alfayo:** **(clearing throat)** Samahani, tafadhali tunaweza kuagiza vinywaji? Glasi moja ya *white wine...* na mimi nitakunywa ehhh, mvinyo mkali *whisky*."

**5a. Waiter:** Hakuna shida!

**6. Jennifer:** Alfayo! Mara moja hii umeanza kunywa whisky! Watu watafikiria unataka ujasiri wa Kiholanzi! Je kuna kitu unataka kuniambia? Si kawaida yako! **(chucking)** Sasa … ehhhhh, nafikiri nitakula pilau ya kuku.

**7. SFX:** **Putting glasses on table**

**8. Waiter:** Vinywaji tayari! Je, mko tayari kuagiza chakula ?

**9. Alfayo:** Subiri kidogo. Asante… **(taking huge gulp of whisky)** Jennifer ama kwa hakika, kuna kitu muhimu ningependa kukwambia. Lakini kwanza endelea kupata kinywaji kabla kukueleza niliyo nayo moyoni.

**10. Jennifer:** Sawa… Nilijua tu mualiko wako si bure, kuna kitu unataka kuniambia. **(getting nervous)** Niambie tu Alfayo. Ni nini? Kwani umepata mpenzi mwengine? **(pauses and waits for a response, but there is none. Alarmed:)** Alfayo? Huuuh, Una mpenzi mwengine?

**10. Alfayo:** **(choking on drink and laughing)** Sina! Sina, si hayo ninayotaka kukwambia.

**11. Jennifer:** Uuugh,afadhali! Sasa ni nini kinachokusumbua kama sio masuala ya mapenzi? Unaonekana na wasiwasi sana?

**12. Alfayo:** **(softly spoken, almost whispering during the whole "confession")** Ni kuhusu sakata inayozunguka sekta ya nishati. Miezi michache iliyopita, nilipokea simu kutoka kwa Bw. Mwichuli. Sikuwa na habari kwamba ni mwandani wa karibu wa waziri wa nishati, John Maina.

**13. Jennifer:** **(also in a low voice during this conversation)** Hivi ni kwa nini walikupigia?

**14. Alfayo:** Inaonekana sababu kubwa ya kustawi kwa kampuni yangu katika muda wa miaka michache iliyopita, ilitokana na kuuza vifaa vya umeme kwa kampuni bandia, kampuni ambazo haziko!

**15. Jennifer:** **(louder)** Kampuni ambazo haziko? Unamaanisha nini?

**16. Alfayo:** **(quietly)** Sssssh…Hivyo ndivyo walaghai kwenye sakata wamekuwa wakiendesha shughuli zao. Kuna hizi kampuni bandia zinazodaiwa kuuza umeme kwa taifa, ambazo hazina umeme huo wala kuhusika na kazi hiyo, kwasababu hazina vituo vya kuzalisha umeme. Na kupitia madai ya kununua vifaa vya umeme kama vile mita na vifaa vinginevyo, hasa kutoka kwa kampuni kama yangu, zinahadaa umma na serikali kwamba kweli zinasambaza umeme. Kisha baadaye hulipwa mabilioni ya pesa bila ya kufanya chochote. Mara ya kwanza sakata hili lilifichuliwa na Jeffrey wakati alipokuwa bado anahudumu katika Halmahauri ya Kupambana na Ufisadi.

**17. Jennifer:** Kwa hivyo, anafahamu yote kuhusu sakata hili?

**18. Alfayo:** Ndio lakini subiri nimalize kusema. Walinipigia simu kunieleza kile walichodai eti ni habari njema kwamba kiwango cha mauzo ya mita zangu kwa kampuni hizi bandia kimeongezeka. Lakini nikakataa kandarasi hizo baada ya kugundua kwamba kampuni hizi ni za uongo, na vifaa ninavyowalisha huishia kwenye ghala, huku, waziri wa nishati na walaghai wenzake wakiendelea kujitajirisha kupitia kandarasi bandia wanazotoa kwa kampuni.

**19. Jennifer:** Hii ndio sababu biashara yako imekuwa ikiimarika ghafla? Kumbe ni sehemu ya sakata hili katika sekta ya nishati. Sivyo?

**20. Alfayo:** Ndio. **(still speaking quietly, but insistent)** Lakini nataka unielewe Jennifer - Sikuwa na habari kwamba nahusishwa katika sakata hili. Ninavyoelewa ni kwamba nimekuwa nikiuza bidhaa zangu kwa kampuni halali. Na nilikuwa na anwani, na taarifa zote za benki. Isitoshe wamekuwa wakinilipa bila kuchelewa kumbe ni pesa zinazotokana na visa vya uhalifu. Hii ni njama ya mtandao wa visa vya ufisadi vinavyodidimiza nchi hii kiuchumi. Niliwambia kwamba kamwe sitaki tena kuhusika na biashara hiyo.

**21. Jennifer:** Umefanya vizuri sana. Lakini Alfayo- hii ina maana kwamba moja kwa moja wewe ni mhusika katika sakata hili? Na endapo itafichuliwa, huoni kwamba pia wewe utakuwemo mashakani? Hawa wanasiasa wanataka mtu watakaye mtumia kama chambo, na hapana shaka wewe ndiye utakuwa chambo hicho!

**22. Alfayo:** Nafahamu hilo. Ndio sababu nikaamua kujitokeza hadharani kusafisha jina langu. Nimezungumza na Jeffrey na watu wake kutoka shirika la "Komesha Ufisadi sasa." Nitaenda rasmi kutoa ushahidi mbele ya kikosi kazi. Wanahitaji shahidi ambaye anafahamu kwa kina sakata hili ili kusaidia katika kuwafichua walaghai na yote yanayoendelea katika sakata hili, na niko tayari kutoa ushahidi huo wanaoutaka.

***KW Begin***

**23. Jennifer:** Una uhakika unataka kuwa mpuliza kipenga?

**24. Alfayo:** Ndio. Na sina jinsi. Naamini cha msingi ni kujitokeza hadharini na kueleza waziwazi ninachofahamu kuhusu sakata hili. Mimi sikuwa na habari kuhusu sakata hili wakati nikiuza mita hizo. Nadhani wataweza kunielewa kwamba mimi ni fisadi.

***KW End***

**25. Jennifer:** Na je, kuhusu Bw. Mwichuli na wenzake? Huoni wataanza kukuandama? Au kutuandamana kama familia?

**26. Alfayo:** Pengine. Tunaweza kuwa hatarini Jennifer. Lakini najua ninachokifanya. Siwezi kuendelea kuwauzia bidhaa zangu, lakini pindi mambo haya yatakapotokea hadharani, itabainika nani wa kulaumiwa. Wasiwasi wangu ni wewe na wale watoto!.

**27. Jennifer:** Ndio .... ndio ..ndio, pengine … unafikiri ni bora tuhame hapa nchini kwa muda? Hasa wakati habari hizi zitakapoanza kuenea?

**28. Alfayo:** Kwenda wapi sasa? Nimekuwa nikilifikiria sana jambo hili, lakini ni vyema kubakia hapa hapa, bora kuwa waangalifu. Jeffrey amenihakikishia kwamba, punde habari hizi zitakapoenea, shirika lake litatupa ulinzi kwa muda.

**29. Jennifer:** Sasa tuna muda gani? Na ni lini habari hizi zitawekwa hadharani kwenye vyombo vya habari?

**30. Alfayo:** Kabla ya uchaguzi mkuu ujao, tuseme ndani ya muda wa siku mbili.

**31. Jennifer:** **(big gasp)**

**End of Scene One**

**32. Narrator:** Sasa nyavu imeanza kumuandama waziri wa nishati na walaghai wenzake wanaohusika na sakata hili katika sekta ya nishati. Hatimaye, Alfayo amemueleza mkewe Jennifer yote anayofahamu kuhusiana na sakata hili na sasa shirika la kukomesha ufisadi linajiandaa kutoa hadharani habari kuhusu sakata hili. Lakini je, watafaulu kumzuia waziri wa

nishati, John Maina, kuwa Rais. Wakati huo huo,binti wa Alfayo, Lydia na rafiki yake Tekla pia watatekeleza jukumu lao katika kupambana na ufisadi. Wanajaribu kufichua kashfa ya ulaji rushwa shuleni, pia kwa ushirikiano wa shirika la Jeffrey.

**Scene Two:**

**33. SFX:** **Door opens**

**34. Lydia:** **(out of breath)** Sylvia! Tumefaulu! Tumefaulu kurekodi… Ohh, samahani, kuna mkutano unaendelea?

**35. Sylvia:** Sawa, Lydia. Nilikuwa na mkutano kidogo na waandishi wa habari.

**36. Journalist 1:** Unazungumzia kurekodi sauti gani hiyo? Na hawa wasichana ni kina nani, Sylvia?

**37. Sylvia:** Huyu hapa ni dadangu mdogo, Lydia Odhiambo, na rafiki yake, Tekla. Pia wao wana habari wanataka kutueleza. Naamini zitakuwa za manufaa kwenu.

**38. Journalist 2:** Ni kuhusu nini?

**39. Lydia:** Kwanini msiwasikilize? Sylvia, Naweza kuunganisha redio yako kwa spika?

**40. Sylvia:** Sawa – hii hapa.

**41. SFX:** **Connecting recorder to speaker, pressing “play”**

***41. Recorded part from Episode 7 played on recorder:***

***“Oh, Mwalimu Tatu, ama kwa hakika tumekuwa tukilifikiria sana jambo hili tangu ulipotueleza. Je, endapo wazazi wetu watakuwa tayari kukupa kitu kidogo kama ulivyosema, hilo litakuwa tatizo kwako?***

***Hapana, kwa vile nyinyi ndio mnaouliza, hakuna shida kabisa. Sio mimi peke yangu anayechukua pesa, -na tafadhali usiseme ni “hongo” kama ulivyosema wakati ule! Hivyo ni kusema mimi ni mhalifu! (laughs) Pengine tunaweza kusema ni “ada ya kuimarisha alama shuleni” au pesa kidogo za kumsaidia mwalimu"... (laughs)***

***Isitoshe waalimu wengi katika shule zetu hufurahia sana wanapopewa pesa kidogo za kuimarisha matokeo shuleni."***

**42. Journalist 1:** Safi sana hii. Nahitaji nakala yake. Na hakika mhariri mkuu ataipenda! Tunaweza kuitumia katika taarifa zetu za jioni?

**43. Journalist 2:** Mimi pia.

**44. SFX:** **Door opens**

**45. Jeffrey:** **(door closing)** Kunaendelea nini hapa, Sylvia?

**46. Sylvia:** Lydia na Tekla wamerudi sasa hivi na baada ya kumrekodi mwalimu wao akikiri kujihusisha na rushwa shuleni. Ni moto wa kuotoea mbali.…

**47. Jeffrey:** Na kwanini umewaruhusu waandishi wa habari kuisikiliza ripoti hii kabla ya sisi kuichunguza zaidi?

**48. Sylvia:** Ni..ni…nimeonelea bora kazi hii ianze mara moja.

**49. Jeffrey:** Sawa. Kuna mambo kadhaa tunapaswa kujadili kuhusiana na kesi hii. Kwanza: hawa wasichana wawili ni watoto sana, Endapo mtahitaji nakala, basi lazima mweke sahihi fomu ya makubaliano ya kuhifadhi siri. Majina yao hayapaswi kufichuliwa. Tumeelewana?

**50. Journalist 2:** Ni sawa, Jeffrey. Tutafanya hivyo sasa hivi. Hatuwezi kufichua majina yao, tunakuhakikishia hilo!

***KW begin*** Lakini nahitaji nakala hiyo sasa hivi, ili tuweze kuchapisha taarifa hii kwenye gazeti la kesho. Nina saa chache sana kabla ya muda wa mwisho wa kuwasilisha ripoti zetu kumalizika.

**51. Jeffrey:** Sylvia atajaribu kupanga karatasi hizo. Kumbuka endapo majina ya wasichana hawa yatachapishwa, basi tutawachukulia hatua za kisheria. Nadhani tumeelewana.

**52. Journalist 1:** Sawa… Jeffrey, tunaweza kufanya mahojiano mafupi kuhusu matumaini yake katika uchaguzi mkuu ujao? Una imani kwamba utaingia bungeni?

**53. Jeffrey:** Ni matumaini yangu kwamba watu wa nchi hii wanataka kuona ufisadi ukikomeshwa kabisa. Na iwapo wana matumaini hayo, basi lazima wanipigie kura. Samahani sina muda wa kutosha kufanya mahojiano kwa sasa. Lydia na Tekla hebu nifuateni- Nataka kusikiliza kanda hiyo na kisha mnieleze jinsi mambo yalivyokwenda .

***KW end***

**End of Scene Two**

**<u>Scene 3 :</u>**

**54: SFX:** ***Beep - beep - beep*** **[Radio news opener]**

**55. Newsreader on the radio:** Hii ni taarifa ya habari ya saa Tatu. Waziri wa elimu ametangaza uchunguzi wa kina ufanywe kuhusiana na madai ya kuenea kwa visa vya ulaji rushwa katika shule za humu nchini. Akizungumza nje ya ofisi yake leo jioni, waziri alisema kuwa ni jambo lisilokubalika kwa mwalimu yoyote kula rushwa ili kumsaidia mwanafunzi katika matokeo yake ya mtihani. Taarifa hii imetokea baada ya wanafunzi wa shule ya sekondari kunasa sauti ya mwalimu akikiri kula

rushwa mara kadhaa, ili kuwasaidia wanafunzi kupata matokea bora katika mitihani wao…. **(fade out)**.

**MUSIC (FADE UNDER OUTRO)**

**54. Narrator:** Na hadi hapo msikilizaji tunafika mwisho wa kipindi cha leo **Noa bongo jenga maisha yako**, ikiwa ni sehemu ya nane ya mfululizo wa mchezo kuhusu Ufisadi kwa jina -**Tembo Nyumban**i . Huku kashfa za ulaji rushwa zikiendelea kufichuliwa, mchecheto wa kisiasa unazidi kukumba nchi hiyo wakati uchaguzi unapokaribia. Je, Jeffrey Thiongo ana nafasi gani ya kuingia bungeni? Kwa upande mwengine, Alfayo Odhiambo, anajiandaa kukabiliana na vita baada ya kukataa ombi kutoka kwa walaghai na badala yake kupuliza kipenga cha ufisadi dhidi ya waziri wa nishati. Ungana nasi kwenye kipindi kinachofuata katika mchezo huu wa redio ili upate kufahamu mengi zaidi. Ukiwa ungependa kukisikiliza tena kipindi hiki tembelea mtandao wetu wa dw.de/lbe. Au ukiwa na maoni usisite kututumia kupitia ukurasa wetu wa Facebook. Hadi wakati mwengine. Kwaheri na asante kwa kutusikiliza!